# UTANGULIZI

Tume ya Pamoja ya Fedha ni Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 134 na kuanzishwa kupitia Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140. Jukumu la msingi la Tume ni kutoa ushauri na mapendekezo kuhusu Uhusiano wa Kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Aidha, Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kupitia Ibara ya 124 inatambua mamlaka ya Tume ya Pamoja ya Fedha kutekeleza majukumu yake Zanzibar. Tume ilianza kutekeleza majukumu yake mwaka 2003.

## MAJUKUMU YA TUME

Majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha yameainishwa katika Ibara 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa mujibu wa Ibara hizo, majukumu hayo ni:

- Kuchambua Mapato na Matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa Mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo wa Serikali hizo;
- Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za kifedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;
- Kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza, na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

## DIRA

Kuwa Taasisi yenye Utalaamu wenye weledi katika kusimamia Uhusiano wa Kifedha kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuimarisha Muungano wa Tanzania.

## DHIMA

Kutoa Ushauri wa Kitaalamu kuhusu Uhusiano wa Kifedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuimarisha na kudumisha Muungano wetu.

## MISINGI YA UTENDAJI KAZI

- Uadilifu
- Weledi
- Ushirikiano
- Ubunifu
- Uwajibikaji

## MUUNDO

Muundo wa Uongozi wa Tume ya Pamoja ya Fedha una ngazi tatu (3). Ngazi hizo ni: Makamishna; Sekretarieti; na Menejimenti.

### Makamishna

Tume inaundwa na Makamishna wasiozidi saba (7) wanaoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa sheria, endapo Mwenyekiti wa Tume atatoka upande mmoja wa Muungano, Makamu Mwenyekiti atatoka upande wa pili wa Muungano.

### Sekretarieti

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140, Sekretarieti inaundwa na:

i) Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);

ii) Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA);

iii) Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) au wawakilishi wao; na

iv) Katibu wa Tume.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, Tume imepewa fursa ya kuteua wajumbe zaidi kwenye Sekretarieti kadiri itakavyoona inafaa. Kwa sasa, wajumbe walioteuliwa wanatoka:

i) Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (SMT); na


iii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (SMZ).

Jukumu la Sekretarieti ni kuwa chombo tendaji chenye wajibu wa kuchambua na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Tume kuhusu masuala mbalimbali ya Uhusiano wa Kifedha kati ya SMT na SMZ.

### Menejimenti

Menejimenti ya Tume inaundwa na wakuu wa Idara, Katibu Msaidizi Ofisi ya Tume Zanzibar na Wakuu wa Vitengo.

## MUUNDO WA TUME YA PAMOJA YA FEDHA




## ORODHA YA MAKAMISHNA WA TUME TANGU KUANZISHWA

### Awamu ya Kwanza (2003 – 2008)

i) Mhe. William H. Shellukindo (Mb) - Mwenyekiti;
ii) Bw. Khamis M. Omar - Makamu Mwenyekiti
iii) Balozi Charles M. Nyirabu- Kamishna
iv) Dkt. Edmund B. Mndolwa - Kamishna
v) Dkt. Hawa Sinare - Kamishna
vi) Bi Amina Zidikheri - Kamishna
vii) Bw. Simai P. Makame– Kamishna

### Awamu ya Pili (2008 – 2013)

i) Bw. William H. Shellukindo (Mb)-mwenyekiti
ii) Bw. Abdulrahman M. Jumbe - Makamu Mwenyekiti
iii) Bw. Khamis M. Omar - Kamishna
iv) Mhe. Othman M. Othman (MBLW) - Kamishna
v) Dkt. Edmund B. Mndolwa - Kamishna
vi) Dkt. Alhj. Juma Ngasongwa – Kamishna
vii) Mhe. Dkt. Pindi H. Chana (Mb) – Kamishna.

### Awamu ya Tatu (2014 – 2019)

i) Bw. Abdulrahman M. Jumbe - Mwenyekiti.
ii) Alhaj Dkt. Juma Ngasongwa - Makamu Mwenyekiti.
iii) Bw. Othman M. Othman - Kamishna.
iv) Bw. Juma A. Hafidh - Kamishna.
v) Bi. Edna N. Nyanguli - Kamishna.
vi) Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (MB) - Kamishna.
vii) Alhaj. Ramadhani M. Khijjah - Kamishna.

## WASILIANA NASI

Barua pepe: katibu@jfc.go.tz
Tovuti: www.jfc.go.tz
Simu: +255-22 2120576

## OFISI ZETU ZINAPATIKANA

Jengo la Sukari (Sukari House)-Mtaa wa Sokoine/Ohio
S. L. P. 9281
DAR ES SALAAM
Jengo la ZSTC-Mtaa wa Gulioni
S. L. P. 1796
ZANZIBAR

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

UHURU NA UMOJA

## TUME YA PAMOJA YA FEDHA

# MAELEZO MAFUPI KUHUSU TUME YA PAMOJA YA FEDHA